

**HOTUBA YA MKUU WA MKOA WA RUKWA MHE.
MAGALULA SAID MAGALULA ALIYOITOA WAKATI WA
KIKAO KAZI NA WAFANYABIASHARA WA MJINI
SUMBAWANGA KATIKA UKUMBI WA LIBORI CENTRE
SUMBAWANGA TAREHE 03 JANUARI, 2016**

Mwenyekiti wa TCCIA - Mkoa wa Rukwa,
Katibu Tawala Mkoa,
Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya ya Sumbawanga,
Ndugu Wafanyabiashara na Wakulima,
Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya ya Sumbawanga,
Mkurugenzi wa Manispaa ya Sumbawanga
Viongozi wa Taasisi za Serikali,
Watendaji wa Serikali,
Ndugu Waandishi wa Habari
Wageni waalikwa
Mabibi na Mabwana.

Napenda kuchukua fursa hii, kumshukuru Mwenyekiti wa
TCCIA - Mkoa wa Rukwa kwa kuitikia wito pamoja na
Timu nzima ya wafanyabiashara wa Mjini Sumbawanga.

Niliona ni vema tukutane pamoja leo kwa ajili ya kuona namna bora ya kuupeleka Mkoa wetu mbele katika masuala ya uchumi na uzalishaji, hivyo kwa masuala ambayo tutayajadili mahala hapa nitaomba ujumbe wake usambazwe Mkoa mzima kwa ajili ya utekelezaji.

Kama ambavyo amegusia Kaimu Katibu Tawala Mkoa, madhumuni ya kukutana kwetu mahala hapa, ni kwa ajili ya kujadili na kuona uwezekano wa ninyi wafanyabiashara kuitumia fursa ya kuwekeza katika biashara ya uongezaji thamani mazao yanayozalishwa ndani ya Mkoa.

Kikao hiki pia ni muafaka kujadili na kupata ufumbuzi wa masuala mengine ambayo ni kikwazo katika maendeleo ya Mkoa kibiashara.

Serikali inazidi kutoa fursa kwa Sekta binafsi kuweza kutekeleza majukumu yake kwa dhana ya (Public Private Partnership), Serikali ina wajibu wa kuweka mazingira wezeshi kwa Sekta binafsi kuwekeza na kutengeneza faida kwa kufuata miongozo, sheria, kanuni na taratibu.

Ni wajibu wa Serikali kuweka mazingira wezeshi kwa kuwa Sekta binafsi ni mdau muhimu katika Maendeleo kwa kuwa idadi kubwa ya Ajira zipo Sekta binafsi, pia Sekta binafsi ni walipa kodi wazuri na kuwezesha Serikali kutoa huduma kupitia makusanyo ya kodi.

Serikali ina wajibu wa kuhakikisha Sekta binafsi inakuwa endelevu kwa kushirikiana pamoja na Sekta binafsi yenyewe kukabiliana na changamoto mbalimbali zitakazojitokeza ili kuwa na uchumi endelevu.

Hivyo natoa wito kwa Taasisi zote za Serikali pamoja na Wafanyabiashara, kwanza tuone uwezekano wa kufanya kazi pamoja kwa mtazamo chanya, tutambue fursa zilizopo na kuona namna bora ya kuzitumia kwa nguvu ya pamoja, tuainishe changamoto tutakazozibaini na tuone namna ya kuzikabili kwa pamoja.

Tutumie fursa hii vizuri kusikiliza mada itakayowasilishwa kuhusu uzalishaji wetu ndani ya Mkoa na kubaini maeneo ya uwekezaji hususani uongezaji thamani, pia tutapokea mawasilisho ya taarifa ya TCCIA pamoja na mapendekezo

yao ili tuone namna bora ya kutoka hapa tulipo na kusogea mbele kimaendeleo.

Baada ya kusema hayo kwa uchache napenda kusema kikao hiki kimefunguliwa rasmi.

Asanteni kwa kunisikiliza.

Magalula S. Magalula

MKUU WA MKOA

RUKWA